

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Telegram: **"UVUVI"**
Simu: +255 262322612
Fax: +255 262322613
E-Mail: ps@uvuvi.go.tz
E-Mail: ps@mifugouvuvi.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S. L. P. 2847,
DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Dodoma Desemba 31, 2022

**UFAFANUZI KUHUSU KUSITISHWA KWA MATUMIZI YA TAA ZA SOLA
KATIKA UVUVI WA DAGAA ZIWA VICTORIA**

Ndugu Waandishi wa Habari,

Hivi karibuni kumekuwepo na Taarifa inayozunguka kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu kusitishwa kwa matumizi ya Taa za Sola katika uvuvi wa Dagaa kwenye Ziwa Victoria. Taarifa hiyo ilieleza uwepo wa Agizo la Serikali la kusitisha Uvuvi wa Dagaa kwa kutumia Taa za Sola zinazotumia betri za pikipiki ifikapo tarehe 1 Januari 2023. Pia taarifa hiyo iliainisha malalamiko kuwa Taa za sola zinazodaiwa kupendekezwa zinazuzwa kwa bei ghali ambayo wavuvi hawawezi kuzimudu kutokana na kipindi kifupi kilichotolewa kusitisha matumizi hayo.

Ndugu waandishi wa habari,

Kutokana na taarifa hiyo, napenda kutumia fursa hii kutoa ufafanuzi wa kitaalam kwa Umma ili kuondoa sintofahamu iliyoanza kujengeka miongoni mwa jamii hususan wavuvi katika Ziwa Victoria.

Ndugu waandishi wa habari,

Ifahamike kuwa, Nchi yetu inaongozwa na Sheria zinazotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi nchini unaongozwa na Sheria zilizopo. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Sekta ya Uvuvi pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kulinda, kuendeleza, kusimamia na kuhifadhi raslimali za uvuvi nchini ili ziwe endelevu kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Ibara ya 27 na 28.

Vilevile, Usimamizi wa Raslimali za uvuvi Nchini unazingatia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015; Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2018, 2019, 2020 na 2022. Aidha, Kwa upande wa uvuvi wa dagaa vigezo na masharti ya uvuvi huu yapo katika Kanuni ya 66 ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na Marekebisho yake kuhusu matumizi ya taa za sola katika shughuli za uvuvi.

Ndugu Waandishi wa habari,

Baada ya maelezo haya ya Utangulizi naomba kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Moja, Serikali haijatoa Agizo la ukomo wa matumizi ya Taa za Sola kama ilivyodaiwa. Hata hivyo, Wizara kupitia Mkutano wa wadau wa Sekta ya Uvuvi uliofanyika mwezi Novemba 2022 mkoani Mwanza pamoja na masuala mengine ulijadili suala hili na kuazimia kuanza kutolewa kwa Elimu kuhusu matumizi sahihi ya Taa za Sola kwa kushirikiana na wadau. Azimio hili limeanza kutekelezwa na ni suala endelevu hata hivyo kumekuwepo na upotoshaji wakati wa zoezi hili. Wizara itaendelea kusimamia kwa ukaribu na kuchukua hatua stahiki ili kuondoa upotoshaji unaoendelea kujitokeza.

Ndugu waandishi wa habari,

Nachukua fursa hii, kuhimiza wavuvi wote hususan wa Dagaa Ziwa Victoria na wananchi kwa ujumla kuendelea na shughuli zao za uvuvi kwa kutumia zana na njia rafiki ili kulinda raslimali za uvuvi, Ikolojia na mazingira kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Pili, napenda kueleza kuwa Serikali ina utaratibu wa wazi kuhusiana na masuala ya msamaha wa Kodi na Ruzuku. Hivyo, Wizara itaendelea kufuata utaratibu huo ili kuona uwezekano wa kutekeleza hoja husika. Aidha, nitumie fursa hii kuhimiza wadau wote wa suala hili wakiwemo watoa huduma wa Taa za Sola kufuata utaratibu uliopo kuhusu masuala ya kikodi.

Tatu, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi (Biashara huria) na kwamba kila mdau mwenye nia ya kuwekeza katika fursa mbalimbali zinazojitokeza kwenye Sekta ya Uvuvi kufanya hivyo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Nne, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ilifanya utafiti kwa kutumia taa za aina zote zinazotumika kwenye uvuvi husika, ikijumuisha na zile zinazoendeshwa na betri za pikipiki na zinazoendeshwa na mafuta ya taa (karabai) ambapo ilipendekeza kutumika kwa taa za sola zenye jumla ya Watt 90 kwa chombo cha uvuvi, kwa maana ya kwamba kila taa moja isizidi Watt 10.

Vilevile, taarifa za kitafiti zimethibitisha kwamba betri zenye kutumia teknolojia ya '**lead-acid**' (betri za pikipiki) zinasababisha uchafuzi wa mazingira, hasa zinapotumika vibaya na kutupwa kwenye maji hivyo kuwa na uwezekano wa kuharibu ikolojia na mazingira ya ziwa.

WITO KWA WAVUVI NA WANANCHI KWA UJUMLA

Ndugu Waandishi wa habari,

Nahimizia wadau wa uvuvi kuendelea kufanya uvuvi endelevu na kwa wavuvi wa Dagaa kuzingatia Sheria zilizopo ili kuepuka uharibifu wa mazingira, athari kwa bioanuai na Ikolojia kwa mazalia ya samaki na mazingira kwa ujumla. Aidha, nahimiza watu wote kuzingatia taratibu za kupata taarifa kutoka vyanzo vya uhakika vya Serikali kabla ya kutoa taarifa zenye kuleta taharuki kwa jamii.

Asanteni kwa kunisikiliza

Imetolewa na
Bw. Magese Emmanuel Bulayi
MKURUGENZI WA UVUVI
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
31 DESEMBA 2022